

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017 KUISHIA JUNI, 2017 KWA
MIRADI YA MAENDELEO

1.0 UTANGULIZI

Halmashauri wilaya ya Lushoto ina ukubwa wa Kilometa za Mraba **2,300** na imepakana na Nchi ya Kenya kwa Upande wa Kaskazini Mashariki, Mkoa wa Kilimanjaro kwa Upande wa Kaskazini Magharibi, Halmashauri ya Bumbuli upande wa Kusini, Wilaya ya Korogwe kwa upande wa Magharibi na Wilaya ya Mkinga kwa Upande wa Mashariki. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo 4° 25' – 4°55' Kusini mwa Ikweta na Longitudo 30° 10' – 38° 35' Mashariki mwa Greenwich.

1.1 HALI YA HEWA

Wilaya ya Lushoto inapata kiasi cha wastani wa mm800 – mm2000 za mvua katika ukanda wa Milimani kwa mwaka na Ukanda wa Tambarare wastani wa mvua kwa mwaka ni mm 500 – 800. Kwa ujumla Wilaya yetu ina misimu mikuu mitatu ya hali ya hewa:-

- (i) Msimu wa Vuli (Kuanzia mwezi Oktoba – Februari)
- (ii) Msimu wa Masika (Kuanzia mwezi Machi – Juni)
- (iii) Msimu wa Kipupwe (Julai – Septemba).

1.2 UTAWALA NA MAKAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ina jumla ya Tarafa 5, Kata 33, Vijiji 125 na Vitongoji 954. Aidha Halmashauri ina Majimbo 2 ya uchaguzi ambayo ni Lushoto na Mlalo. Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka 2012, Wilaya ya Lushoto ilikuwa na watu **332,436** kati yao Wanaume ni 153,847 (46%) na Wanawake 178,589 (54%). Kulingana na kasi ya ongezeko la watu la asilimia 1.1 kwa mwaka, Wilaya kwa sasa inakadiriwa kuwa na watu 350,720 kati yao Wanaume ni 161,331 na Wanawake ni 189,389 ambapo msongamano wa watu umefikia Wastani wa watu 146 kwa kila kilometa ya Mraba.

1.3 HALI YA KISIASA

Hali ya kisiasa ni nzuri. Chama Cha Mapinduzi na Vyama vyote vinashirikiana kwa ukaribu na serikali, katika mustakabali wa maendeleo ya Wilaya. Idadi ya vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu vilivyopo katika Wilaya ni nane 8 navyo ni CCM, NCCR Mageuzi, UMD, ACT-WAZALENDO, CUF, CHADEMA, TLP na APPT Maendeleo.

1.4 HALI YA UTUMISHI

Wilaya ina jumla ya Watumishi wa Serikali **3221** kati ya Watumishi 4,014 wanaohitajika katika kada mbalimbali, hii ni sawa na asilimia **80.2** ya watumishi waliopo na kufanya upungufu kuwa ni sawa na asilimia **19.8**.

MCHANGANUO WA MPANGO NA MTIRIRIKO MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/2017

Jedwali Na. 1

Na	Maelezo	Bajeti	Fedha Pokelewa na Kutumika	% ya mapokezi
1	Mfuko wa barabara (Road Fund)	1,491,730,000	1,381,022,659	92.58%
2	Ruzuku ya maendeleo (LGCDG)	1,196,477,000	418,388,000	34.97%
3	TASAF	70,950,000	2,175,332,020	3066.01%
4	NRWSSP	211,682,000	713,965,195	337%
5	Tao la Mashariki (EAMCEF)	13,200,000	8,600,000	86.04%
6	Mfuko wa Majimbo	80,601,000	78,700,000	97.64%
7	SEDP (ADB)	578,164,001	0	0%
8	PEDP(WB)	100,000,000	0	0%
9	MMAM(HSD)	141,050,000	0	0%
	Jumla	3,883,854,001	4,776,007,874	122.97%

Mapato ya ndani

Na	Maelezo	Bajeti	Fedha Pokelewa na Kutumika	% ya mapokezi
1	Mapato ya ndani	2,060,420,300	1,957,399,285	95%

2.1 Utekelezaji wa miraji ya maendeleo linganifu na Bajeti na mapokezi ya fedha. MIRADI MIPYA - 2016/2017

Jedwali Na. 2

1. MAJI

	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Mradi wa usambaji wa maji Irente	Mradi umekamilika
2	Mradi wa usambazaji wa maji Kivingo	Mradi umekamilika
3	Mradi wa usambazaji wa maji Mlalo/Mwangoi	Mradi umekamilika
4	Mradi wa usambazaji wa maji Mloa/Lwandai	Mradi umefikia 85% ya utekelezaji
5	Mradi wa usambazaji wa maji Ngulu	Mradi umefikia 50% ya utekelezaji.
6	Mradi wa usambazaji wa maji Shume/Manolo/Madala	Mradi umefikia 20% ya utekelezaji
7	Mradi wa usambazaji wa maji Gologolo	Mradi upo kwenye hatua za awali za utekelezaji. Utekelezaji upo kwenye 10%

2. MALIASILI - EAMCEF

	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Utoaji wa vibali na ufuatiliaji	Vibali tuna toa kwa watu wenye miti kwenye mashamba yao. Tulifuatilia miti iliyoombwa kwa ajili ya madawati na ujenzi wa Nyumba ya mwalimu kata ya Mlola. Tulifuatilia kibali tulicho toa kwa chuo cha mabughai,
2	Uharibifu wa mazingira kijiji cha Kinko na Nkundei	Tuli waelimisha viongozi wa vijiji kutumia sheria Ndogo zilizopo kwa kuwa adhibu watu wanao lima kwenye vilele vya milima.
3	Ukaguzi wa mazao ya misitu na ukusanyaji wa ushuru kituo cha Nyasa.	Ushuru na ukaguzi wa mazao ya misitu bado unaendelea Jumla ya Tsh 87,149,000/= zilikusanywa .
4	Kufanya Doria	Tulifanya Doria ya kwenye maeneo ya Lukozi,Kwemakame,Mlalo na tulifanikiwa kupata jumla ya Tsh 1,274,000/= Mwezi wa Tatu-wa sita 2017, shughuli hii ili kwama kutokana na mvua zilikuwa ni nyingi ili kua nvigumu kupitisha Gari kwenye njia za vichochoroni.
5	Bustani ya miti	Tumeanzisha bustani ya miti hadi sasa ina miche ya miti 1,700 na tunategemea kupatiwa fedha na Halmashauri yetu,hivi karibuni ili tutimize lengo la kukuza miche 20,000 kwa kila msimu wa mvua
6	Kutoa elimu ya uanzishaji wa bustani za miti na ufuatiliaji.	LAC na Wataalam wa Idara tuli fanya ziara ya kukagua na kutoa ushauri kwenye bustani za miti zinazo fadhiliwa na EAMCEF kwenye vijiji vya Ndabwa,Hemboye na Manolo.
7	Upandaji wa miti	Tulipanda miti kwenye wiki ya upandaji miti kuanzia kwesimu-Ubiri, Halmashauri mpya-Maguzoni-Irente , vyanzo vya maji , Mashule , Zahanati, Maeneo ya Dini na Makazi ya watu. Kwa Tarafa zingine miti ilipandwa kwenye maeneo mbalimbali kama Mashule, Vituo vya Afya ,Zahanati, Maeneo ya Dini , makazi ya watu , mashambani . Mvua zinaendelea

		kunyesha watu bado wana panda miti ifikapo July tutaweza kupata Idadi ya miti iliyopandwa na kukua.
8	Kuwezesha vijiji vya Kinko,Kunde ,Migambo na Mavumo kutambua watu wenye mashamba ya nayo pakana na msitu wa magamba asilia	-Wakulima wapatao miambili 200 wametambuliwa na kupatiwa mafunzo ya uanzishaji wa bustani za miti kwa lengo la kupanda miti kwenye mashamba yao ili wasitegemee msitu.Kuunda vikundi vya upandaji miti vinavyo fadhiliwa na mfuko wa hifadhi ya milima ya Tao la Mashariki. -Kuimalisha vikundi vya upandaji miti kwenye vijiji vya Ndabwa,Hemboye na Manolo.

3.1 MAENDELEO YA JAMII - TASAF

	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Uhawilishaji fedha kwa kaya maskini	Kaya maskini 6,826 zimenufaika kwa kupatiwa ruzuku

3.2 MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA

NA	JINA LA KIKUNDI	KIASI KILICHOTOLEWA KWENYE KIKUNDI
1	JITEGEMEE MNAZI	2,000,000
2	UPENDO VITI	2,000,000
3	SUBIRA GOLOGOLO	2,000,000
4	INTERFAITH	2,000,000
5	TAFAKARI	2,000,000
6	UPENDO MSALE	2,000,000
7	UPENDO UBIRI	2,000,000
8	UMOJA KILANGA	2,000,000
9	UJAMAA MAGAMBA COAST	2,000,000
10	KITALA GROUP	2,000,000
11	KIWAMANI GROUP	2,000,000
12	JIKWAMUE VIJANA KWEULASI	2,000,000
13	KIFARU GROUP	2,000,000
14	MKOMBOZI DULE	2,000,000
15	NYOTA NJEMA	1,000,000
16	MAISHA	2,000,000
17	JITEGEMEE	2,000,000
18	JITIHADA	1,000,000
JUMLA		34,000,000

4 BARABARA – ROAD FUND

NA	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Matengenezo ya kawaida barabara ya Malibwi-Kwekanga 8km	Kazi imekamilika
2	Matengenezo ya kawaida barabara ya Mtae-Kweshindo 8.1km	Kazi imekamilika
3	Matengenezo ya kawaida barabara ya Boheloi-Gare 4km	Mkandarasi amepatikana
4	Matengenezo ya kawaida barabara ya Ubiri-Miegeo-Magunga 6km	Kazi imekamilika
5	Matengenezo ya kawaida barabara ya Ngwelo-Kigulunde 8km	Mkandarasi amepatikana
6	Nyasa-Hemtoye-kwekanga 11km	Kazi imekamilika
7	Matengenezo ya kawaida barabara ya Kwekanga-Ngwelo 6km	Kazi imekamilika
8	Matengenezo ya kawaida barabara ya Lunguza-Tewe 13km	Kazi inaendelea
9	Matengenezo ya kawaida barabara ya Viti-Gologolo-Manolo 12km	Kazi imekamilika
10	Matengenezo ya kawaida barabara ya Manolo-Mamboleo-Mambo 11km	Kazi imekamilika
11	Matengenezo ya kawaida barabara ya Mkatoni-Kinko-Kireti-Kwai 15km	Kazi imekamilika
12	Matengenezo ya kawaida barabara ya Kizara - kwemashai 7km	Kazi inaendelea
13	Matengenezo ya kawaida barabara ya Majulai-Mlesa 5km	Kazi inaendelea
14	Matengenezo ya kawaida barabara ya Mlalo-Ngwelo-Mlola 8km	Kazi imekamilika
15	Matengenezo ya kawaida barabara za Lushoto mjini 10km	Kazi imekamilika
16	Matengenezo ya kawaida barabara ya Goka-Dule M 3.4km	Kazi imekamilika
17	Matengenezo ya sehemu korofi barabara ya Mlalo-Ngwelo-Mlola 4km	Kazi imekamilika
18	Matengenezo ya sehemu korofi barabara ya Lushoto mjini 10km	Kazi imekamilika
19	Matengenezo ya sehemu korofi barabara ya Kwekanga-Mlola 1km	Kazi imekamilika
20	Matengenezo ya sehemu korofi barabara ya Mnazi-Mbaramo 3km	Kazi inaendelea
21	Matengenezo ya muda maalumu barabara za Lushoto mjini 12km	Kazi imekamilika
22	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Mnazi-Mbaramo 6km	Kazi inaendelea
23	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Goka-Dule	Kazi inaendelea

	M 6km	
24	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Mtae-Kweshindo-Mnazi 14km	Kazi imekamilika
25	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Malibwi-Kwekanga 6km	Kazi imekamilika
26	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Viti-Gologolo-Manolo 6.2km	Kazi imekamilika
27	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Lunguza-Tewe 5km	Kazi inaendelea
28	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Dochi-Yoghoi 3km	Kazi imekamilika
29	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Mazumbai - Ntambwe - Baga 3km	Kazi imekamilika
30	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Mshizii-Boheloi 3.5km	Kazi imekamilika
31	Matengenezo ya muda maalumu barabara ya Dochi-Gare 3km	Kazi imekamilika
32	Matengenezo ya lami Lushoto mjini	Kazi ipo hatua ya kusaini mkataba
33	Ujenzi wa makalvati	Kazi inaendelea
34	Matengenezo ya daraja la Kibomboi	Kazi inaendelea
35	Gharama za mafuta,matengenezo ya magari na posho za usimamizi	Kazi inaendelea
	JUMLA	

5 RUZUKU YA MAENDELEO – LGCDG

NA	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Ujenzi wa ofisi ya kata ya shume	Ujenzi unaendelea
2	Umaliziaji wa ofisi mbili za kata ya Manolo ya Mng"aro	Umaliziaji unaendelea
3	Kuwezesha kulipa deni la Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la utawala	Jengo limekamilika na linatumika ila bado mkandarasi anatudai jumla ya 1.1 bilioni.
4	Umaliziaji wa ujenzi wa eneo la wazi Nyerere square	Ujenzi unaendelea
5	Kuwezesha umaliziaji wa madarasa 16 kwenye shule za Msingi za Langoni, Nkundei, Makanya, Mboghoi, Kwedau, Nkukai, Mbaru, Kwemashai U, Shwaghoi, Fufui na Lokome	Miradi hii imekamilika
6	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya mwalimu S/M Hondelo	Ujenzi unaendelea
7	Kuwezesha umaliziaji wa nyumba za walimu kwenye S/M za Hemkeyu, Nkombo, Kigulunde N, Makanya, Kwedau, Kwemshazi, Mboghoi, Mpanga, Mtii, Kishangazi, Kwemtindi, Kwemashai, KigulundeN, Nkundei, Madala na Kwekanda.	Miradi hii imekamilika, fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata.
8	Kuwezesha ujenzi wa choo cha wanafunzi matundu 20 kwenye S/M za kibomboi na Gare B	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata

9	Kumaliza ujenzi wa vyoo vya wanafunzi matundu 30 kwenye S/M za Lewa, Mtae and Mng'aro.	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
10	Kumaliza ujenzi wanyumba za walimu kwenye S/S za Ndurumo(1), Ngwelo(1), Shambalai(1) na Shume(1).	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
11	Kumaliza ujenzi wa madarasa 5 kwenye S/S za Lushoto, Kwemaramba(1) na Masange(1)	Project on progress
12	Kuwezesha ujenzi wa mfereji wa kituani Menzae irrigation wenye urefu wa 3000m	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
13	Kuwezesha umaliziaji wa soko la mnada wa mifugo kwenye kata ya Malindi.	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
14	Kuwezesha umaliziaji wa zahanati ya kijiji cha Mbelei	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
15	Kukamilisha ujenzi wa OPD kwenye zahanati za Mazumbai na Mbwei	Miradi hii inaendelea na fedha zilipelekwa kwenye ngazi ya kata
16	Kuwezesha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.	Utekelezaji umefanyika kila robo ya mwaka.

6 MFUKO WA JIMBO

NA	Jina la Mradi	Hatua ya utekelezaji
1	Uchocheaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika ngazi ya kata kwenye kila Jimbo.	Fedha zote zimepelekwa kwenye akaunti za kata na tayari utekelezaji unaendelea

3.0 MAFANIKIO

Pamoja na mafanikio katika ngazi ya kiidara lakini Halmashauri imefanikiwa kufikia lengo la makusanyo ya ndani iliyojiweka ambapo hadi tarehe 31 Mei 2017 tayari ilikuwa imefikia asilimia 95% ya lengo la kukushanya Tsh.2,060,420,300.

Idara ya maendeleo ya jamii

- Kwa mwaka wafedha 2016/2017 Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo kwa wanawake na jumla ya wanawake 40 wamenufaika na mikopo hiyo
- Halmashauri imetoa mafunzo ya ujasiriamali na utatuzi wa migogoro katika vikundi kwa vikundi vya wanawake 69.
- Wanawake waliojengewa uwezo, wameimarisha uwezo wa kufanya biashara ndani na nje ya halmashauri mfano Korogwe, Handeni, Tanga, Dar es salam, Zanzibar, Kilimanjaro na Arusha na nchi jirani ya Kenya.
- Wanawake waliopewa mikopo wameimarisha uwezo wa kusimamia shughuli za uzalishaji kwa kipindi chote cha mkopo na baada ya mkopo
- Tangu mwaka wa fedha 2014/2015 na 2016/2017 jumla ya vikundi kumi na saba (18) vya vijana wamepatiwa mikopo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za kijasiriamali.
- Vijana zaidi ya mia moja (100) kutoka katika vikundi 17 wamenufaika kwa kuanzisha biashara ndogondogo za kuuza nafaka, biashara ya duka, kununua bodaboda na kilimo.

- Pia katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 30 katika kata ya Lunguza kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa vijana. Vijana 26 mpaka sasa tayari wameanza shughuli za kilimo cha vitunguu katika eneo hilo na kwa kuanza wamelima ekari kumi (10). Halmashauri imetoa shilingi milioni kumi (Tshs 10,000,000/=) kwa vijana hao ili kununulia pembejeo za kilimo na kufanikisha gharama za kilimo.
- Walengwa katika Kaya masikini wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (iCHF) na Kaya 3486, zenye wanufaika 7,854 ME. 3,156 na KE. 4,698 wamejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya.
- Kaya maskini zimeweza kupata uhakika wa kupata milo angalau mitatu kwa siku
- Mahudhurio ya watoto shuleni yameongezeka kwa 80%
- Mahudhurio ya kliniki kwa watoto chini ya miaka mitano yameongezeka 80%
- Idadi ya walengwa 5,964 wanajishughulisha na shughuli za ufugaji wa kuku, Bata, Mbuzi na Kodo.
- Jumla ya Kaya 4889 zimeweza kuboresha makazi yao kwa kununua mabati na kununua samani za nyumbani.
- Idadi ya Kaya 158 zimeweza kuunda vikundi na Idadi ya Kaya 431 zimeweza kuanzisha vikundi vya kuweka na kuwekeza.

Idara ya Ardhi na Maliasili

- Upimaji wa viwanja kwa matumizi mbalimbali, viwanja 114 vya Giraffe, vimeandaliwa mchoro wa mipango miji na kuizinishwa Wizara ya Ardhi na Makazi. Upane wa maeneo ya Bara, Bomani, Kitopeni, viwanja 57 vimetambuliwa na kuchukuliwa vipimo vya viwanja hivyo na mchoro wa mpango mji unachorwa.
- Ukusanyaji wa Maduhuli ya serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017 kitengo cha ardhi kimekusanya jumla ya shilingi 30,000,000/=, Demand note 200 zimesambazwa kwa wadaiwa sugu
- Utayarishaji wa Hatimiliki za viwanja kwa Wananchi walioleta maombi yao unaendelea na hati 19 zimeidhinishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi kanda ya Kaskazini.
- Upimaji wa viwanja vya makazi na matumizi mengine katika kijiji cha Lunguza, Upimaji wa viwanja 1,500 vya matumizi mbalimbali unaendelea shughuli ikitekelezwa na wataalamu wa Idara ya Ardhi kwa kushirikiana na wataalamu wa TAMISEMI.
- Utatuzi wa mgogoro wa Ardhi huko Mlalo kati ya kijiji cha Handei na Ngazi, Mikutano ya utatuzi wa mgogoro kati ya wananchi wote umeshafanyika. Mapendekezo ya utatuzi huo yameshapitishwa na Baraza la madiwani la mwezi Mei, 2017. Shughuli imekamiliika.
- Uhamasishaji na upimaji shirikishi eneo la Kata ya Mlalo na Kwemshasha, Wataalamu wamekwenda kuhamasisha na kujibu baadhi ya maswali ya wananchi kuhusu upimaji wa Ardhi na sheria za Ardhi. Na pia wamekubali kupima.
- Utoaji wa hati za kimila kwa wakulima wadogo wa Lukozi (Usambara Lische Trust) na zoezi la valuation kwa nyumba na Ardhi zao. Hati zimeshakamilika na wamepewa, valuation ripoti

imeshakamilika na vyombo vya fedha (Bank ya wakulima) wamepewa mikopo kuwainua kiuchumi.

- Upimaji maeneo ya Masoko, mnadana ofisi. Maeneo ya soko la mbogamboga, mnada kata ya Malindi imepimwa. Pia eneo la kutupa takataka huko Kwai na Soko la Kwemakame.

Idara ya Elimu

- Idara imelenga kuhamasisha wadau mbalimbali kufanikisha uchangishaji wa shule mpya zenye kidato cha tano na sita, na shule hizo ni Mlongwema, Rangwi, Ubiri, na Kwemaramba.
- Upatikanaji wa madawti kwa shule zote za sekondari za serikari na baadhi ya shule kuna ziada ya madawati.
- Ufaulu wa kidato cha nne umeongezeka toka 30.5% mwaka 2012 hadi kufikia 63.4% mwaka 2016, na kidato cha sita ufaulu ni asilimia 98.7.
- Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 51 mwaka 2012 hadi 69 mwaka 2017.
- Maabara za sayansi zimeongezeka kutoka 09 mwaka 2012 hadi kufikia 13 mwaka 2017.
- Walimu wa sekondari wameongezeka kutoka 661 mwaka 2012 hadi kufikia 820 mwaka 2017 ambapo wilaya imejitosheleza kwa walimu wa sanaa, Walimu wa sayansi wameongezeka kutoka 50 mwaka 2012 hadi 132 mwaka 2017.

Idara ya Afya

- Ujenzi wa stoo ya dawa ya akiba ya wilaya (buffer stock)
- Kupunguza vifo vya akina mama wajawazito kutoka vifo 6 hadi 3 kwa mwaka 2013-2016 na hadi kufikia juni 2017 ni kifo 1 tu kimetokea.
- Kufungua na kupeleka watumishi katika zahanati mbili mpya, zahanati ya Mlesa, Tema na Makanka, zote zimeanza kutoa huduma .
- Kulipa stahili mbalimbali za Watumishi wa Idara ya afya (uniform allowance, extra duty, on call allowance).
- Kupunguza msongamano wa huduma za mama na mtoto kwa kukarabati jingo ambalo halikuwa linatumika na mabadilisha jengo la maktaba kuwa wodi.
- Kutoa chakula kwa wagonjwa wote waliolazwa.
- Kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanyia mapato.
- Kununua mashine kubwa ya kisasa ya ultra – sound.
- Kuongezeka kwa idadi ya vituo vinavyoleta madai ya bima ya afya(NHIF) toka 28 – 31 na mapato toka 53,019,963.00 hadi 62,703,958.00 kwa mwezi.

7 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

- Ucheleweshaji wa fedha hususan fedha za miradi ya maendeleo na baadhi ya miradi kuletwa fedha pungufu linganifu ilivyokuwa imepangwa kwenye bajeti fedha za ruzuku ya maendeleo – CDG ambapo zimeletwa asilimia 34.4% tuu.
- Kutoletwa kwa fedha za miradi ya maendeleo kabisa mfano fedha za SEDP, PEDP na MMAM ambazo zilikuwa zimetekgwa kwenye bajeti hivyo kushindwa kutekeleza miradi hiyo kabisa.
- Muamko mdogo wa wananchi kushiriki na kuchangia nguvu kazi zao kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Vikundi vinavyoomba mikopo ni vingi lakini vinavyopata mkopo ni vichache kwa sababu ya uwezo mdogo wa mfuko.

8 HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

- Kuandika barua wizara ya fedha kwa ajili ya kukumbushia fedha ambazo zimechelewesha na ambazo hazijaletwa kabisa.
- Kuahamasisha wananchi kuchangia miradi ya maendeleo.
- Halmashauri na Serikali kuu ziendeele kuuwezesha mfuko wa Maendeleo ya wanawake, ili wanawake wengi wanufaike na kuinua uchumi wa familia na taifa kwa ujumla.